# Tumia Fursa Tengeneza Biashara

Daudi Lubeleje

TOLEO LA KWANZA, 2019

Hakimiliki © Daudi Lubeleje, 2019
Simu: +255 764 771 298, Baruapepe: dlubeleje9@gmail.com

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuhifadhi, kuchapisha kwa njia ya kielektroniki au mekaniki, kutoa vivuli, kurekodi au kubadili sehemu yeyote ya kitabu hiki kwa njia, namna na mfumo wowote bila idhini ya maandishi kutoka kwa mchapishaji.

Sanifu ya kurasa & jalada:
DL Bookstore, Arusha Tanzania
Simu: +255787163013, Baruapepe: dlbookstore@zoho.com

Chapa:
Beanna Publishers, Morogoro
Simu: +255766770422

ISBN 978 0 7334 2609 4



**SALAMU ZANGU KWAKO**

Habari,

Nafurahi sana kitabu hiki kipo mikononi mwako sasa, sina shaka kabisa utakisoma na kujifunza yaliyomo ndani ya kitabu. Nimeandika kitabu hiki, nikiwa na lengo moja tu, kuamsha hamasa ndani yako uweze kuona fursa zinazokuja kwako na utengeneze biashara. Kitabu hiki kitaondoa kabisa mtazamo hasi uliojengeka kwa wengi kuwa ni ngumu kupata mtaji na kuanzisha biashara. Ujumbe wangu kwako ni TUMIA FURSA TENGENEZA BIASHARA!.

**Daudi Lubeleje**

# YALIYOMO


UTANGULIZI 1

SURA YA KWANZA 3

HALI YA UCHUMI NA MTAZAMO WA VIJANA 3

SURA YA PILI 9

KUTAMBUA/KUTENGENEZA NA KUTUMIA FURSA 9

SURA YA TATU 17

FURSA ZA BIASHARA 17

SURA YA NNE 23

NINI KINAFUATA BAADA YA KUANZISHA BIASHARA? 23

KUHUSU MWANDISHI 35

VITABU VINGINE 36

# UTANGULIZI

Unapolitamka au kulisikia neno fursa ni kitu gani kinakuja kwa haraka katika akili yako?. Kitabu hiki nimeandika ili kiamshe hamasa ndani yako ya kutumia fursa kutengeneza biashara. Si hivyo tu, nimeandika mambo kadhaa ya kukusaidia kukuza biashara yako zaidi.

Watu wengi wameshindwa kutumia fursa zinazokuja kwao wakitupia lawama hali mbaya ya uchumi iliyofanya wakose mtaji au hofu ya kupata hasara. Hiki ni kisingizio cha karne cha watu wasiotaka kubadilisha maisha yao kwa sababu fursa huwa nyingi na biashara hutengenezwa wakati mambo yanapoonwa ni magumu.


Nimejifunza kuwa Mungu huona tofauti kabisa na sisi tuonavyo katika jambo hilo hilo moja. Ikiwa watu wote tutajifunza kumsikiliza Mungu, basi ule mtazamo usemwao wa hali ngumu ya uchumi utaondoka na kufutika.

Hivi wajua fursa haziwezi kwisha? Usipoteze muda kusema huzioni, ila ongeza uwezo wako wa kuziona na kuzitumia. Nimeeleza kitabuni mambo ya kukusaidia kuziona fursa na kisha kuzitumia kutengeneza biashara.

Tunahitaji jambo moja muhimu; uthubutu! Wa kuyavulia maji nguo na kuyaoga. Fursa huwekwa mbele yetu kama vile mtu aandikiwaye chakula mbele yake, kazi huwa ni moja; kunawa na kuanza kula ila jambo la kushangaza twabaki kushangaa na kutokula, tunakuja kushtuka fursa imekwisha pita.

Umewahi kusikia msemo huu *“ukianza kulima usigeuke nyuma?”*. Ulikuwa ukitia bidii na kuondoa uvivu tuwapo shambani tukilima. Ukishatumia fursa kutengeneza biashara, hufuata kukuza hiyo biashara. Katika sura za mwisho za kitabu hiki, nimeeleza kuhusu mambo ya kukusaidia kukuza biashara.

Sasa, niseme karibu twende pamoja katika kurasa zinazofuata!.



# 1

## HALI YA UCHUMI NA MTAZAMO WA VIJANA

Hali ya uchumi hutazamwa tofauti kabisa na haya makundi mawili;

1. Walioko duniani hapa hapa
2. Walioko duniani ila wenyeji wao mbinguni.

Tuone andiko hili; Mwanzo 26: 1- 5, 12 *“[1]Ikawa njaa katika nchi hiyo, mbali na njaa ile ya kwanza iliyokuwa siku za Ibrahimu. Isaka akamwendea Abimeleki, mfalme wa Wafilisti, huko Gerari. [2]BWANA akamtokea, akasema, Usishuke kwenda Misri, kaa katika nchi nitakayokuambia. [3]Kaa ugenini katika nchi hiyo, nami nitakuwa pamoja nawe, na kukubariki, maana nitakupa wewe na uzao wako*

*nchi hizi zote. Nami nitakifanya imara kiapo nilichomwapia Ibrahimu baba yako. [4]Nitazidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, nami nitawapa uzao wako nchi hizi zote, na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia. [5]Kwa sababu Ibrahimu alisikia sauti yangu, akayahifadhi maagizo yangu, na amri zangu, na hukumu zangu, na sheria zangu…[12]Isaka akapanda mbegu katika nchi ile, akapata mwaka ule vipimo mia kwa kimoja, BWANA akambariki"*

Sasa twende taratibu bila haraka.

1. Ikawa njaa katika nchi hiyo, mbali na njaa ile ya kwanza. NJAA ni hali ngumu ya uchumi machoni pa watu. Katika kipindi cha Isaka kilitokea kipindi ambacho, kama ni biashara wengine walifunga, watu walikuwa hawana hela, hamna kazi za kufanya. Kila kitu ilikuwa ni NJAA tu. Kama kilimo kiligoma maana hamna mvua, kwahiyo ile chain ya uzalishaji ikaadhirika yote, pengine waliokuwa wameajiriwa wakapunguzwa kazini. NJAA ni kipindi cha ukame, wale wa kulalamika MITAJI hamna waliongezeka na kuzidi sana.

2. *"Isaka akamwendea Abimeleki,...huko Gerari....Bwana akamtokea akasema, usishuke kwenda Misri".* Kwa sababu ya NJAA iliyokuwepo, wengine wakafunga biashara maana hali ni mbaya, hata Mzee Isaka naye akaingiwa na HOFU ya hali mbaya ya uchumi. Kama ilivyo hata leo, kukiwa na hali ngumu, basi utaenda kwa jirani kuomba ushauri, naye Isaka alienda kwa Abimeleki (bila shaka walishauriana kwamba waende Misri) maana watu wote walikuwa wakienda huko. Lakini, je! MUNGU yeye alikuwa akionaje? Wakati watu wote wakiona ile njaa, hali mbaya ya uchumi iliyokuwepo yeye Mungu aliona nini?